Swahili Version

# Mpango wa uhamiaji wa wakimbizi wa Marekani



Ikiwa wewe ni mkimbizi na huwezi rudi nchini mwako unaweza kustahiki kuhamia nchi nyingine. Hii inaitwa *makazi mapya*. Kuhamia nchi nyingine unahitaji kukubaliwa kupitia mchakato rasmi wa usajili. Nchi zote zinazokubali wakimbizi kwa makaazi mapya ina taratibu tofauti ya kupeana makazi mapya.

Nchi ya Marekani ni mojawapo ya nchii duniani ambayo inakubali wakimbizi kwa ajili ya makazi mapya. Tangu 1980, Wamarekani wamepokea wakimbizi zaidi ya millioni 3 kutoka duniani kote kupitia **mpango wa uhamiaji wa wakimbizi marekani au USRAP**.

Kila kesi ya uhamiaji ni ya kipekee na muda unaohitajika kukamilisha mchakato wa USRAP inatengemea hali ya kila kesi. Uhamishaji ni chaguo inayopatikana tu kwa idadi ndogo ya wakimbizi.  Kabla ya kuanza mchakato, ambao utahusisha muda na juhudi kwa upande wako na pia sehemu ya serikali ya Marekani, unapaswa kuwa na uhakika kuwa uko tayari kuhamia Marekani ukipatikana unastahiki.

Ikiwa unachukuliwa kwa ajili ya uhamisho kule Marekani kwa njia ya rufaa na UNHCR ama maombi ya ufikiaji wa moja kwa moja, hatua hizi ni:



## HATUA YA KWANZA: MAHOJIANO KABLA YA UCHUNGUZI

Hatua ya kwanza katika mchakato wa USRAP ni mahojiano kabla ya uchunguzi na kituo cha usaidizi cha uhamishaji au RSC. Serikali ya Marekani inafadhili mashirika ya kimataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali kuendesza kazi za RSCs.

Wafanyakazi wa RSC wataangalia nyaraka zako za kitambulisho na kuunda faili yako ya kesi (na familia yako ikiwa mna jiandikisha pamoja). Picha yako itachukuliwa. Watakuuliza maswali muhimu kuhusu uzoefu wako na kukusanya habari ya kibaografia inayohitajika kwa ajili ya ukaguzi wa awali wa usalama.



## HATUA YA PILI: MAHOJIANO YA USCIS



RSC itawasiliana na wewe kupanga mahojiano na afisa kutoka kwa Huduma za Uraia na Uhamiaji wa Marekani (USCIS) ambayo ni mgawanyiko wa Idara ya Usalama wa Nchi ya Marekani (DHS). Watakuuliza maswali mengi au sawa na ulitojibu kwa mahojiano ya awali ya uchunguzi. Unapaswa kujibu maswali kwa kina na kwa ujuzi wako bora.

USCIS itafanya uamuzi wa mwisho kuhusu kama una stahili kuhamia Marekani.  Wakati RSC inapokea habari kuhusu uamuzi ya kesi yako kutoka USCIS, wata kujulisha:

- Ikiwa wewe na familia yako katika kesi yako mnastahiki kuhamia Marekani;
- Ikiwa wewe na familia yako kwa kesi yako hamustahiki kuhamia Marekani; ama
- Ikiwa USCIS inahitaji muda zaidi kuamua kustahiki kwako.

Ikiwa umejulishwa kuwa kesi yako inastahiki ama kwamba uamuzi ni c utaendelea mbele kwenye mchakato Hata hivyo, *kila kesi iko chini ya kibali cha usalama katika mchakato mzima. Maamuzi ya kesi yanaweza kubadilika wakati wowote*.

**Katika mchakato mzima, maelezo yako yatapelekwa kwa mashirika mengine ya serikali ya Marekani kwa ajili ya hundi za usalama. Mashirika haya huchunguza habari ulizotoa ili kuhakikisha kuwa ni kweli na sahihi. *Wakati mwingine, inaweza kuchukua miezi mingi kukamilisha na, wakati mwingine, huwezi kamwe kupewa na Serikali ya Marekani.***



## HATUA YA TATU: UCHUNGUZI WA MATIBABU

Wewe na kila moja katika familia kwa kesi yako watapangiwa uchunguzi wa matibabu wa lazima. Wakati mwingine uchunguzi wa matibabu utafanyika kabla ya mahojiano yako na USCIS. Tafadhali leta kumbukumbu zote za matibabu na chanjo. Wakimbizi hufanyiwa chanjo kadha kabla ya kuondoka.

## HATUA YA NNE: MWELEKEO WA UTAMADUNI

RSC itapanga uhudhurie mwelekeo wa utamaduni ambapo utapokea habari muhimu kuhusu kusafiri kuelekea Marekani na nini kutarajia unapofika.

Kwa wakati huu, shirika la uhamiaji nchini Marekani litashirikianana na serikali ya Marekani kufanya mipangilio kwa wewe na familia yako ikiwa utaendelea hatua inayofuata ya mchakato. Ikiwa vibali vyote vya usalama vinatolewa, mwisho wa safari yako Marekani utaamuliwa na utakubaliwa kusafiri.





## HATUA YA TANO: SAFARI

Kwa hatua hii, RSC itashirikiana na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji, au IOM, ili kuratibu ndege yako kuelekea Marekani. Unahitaji kutia saini mkopo wa usafiri usio na riba, unaoitwa **Taarifa ya Ahadi**, kulipa gharama ya safari ya ndege. Utahitaji kulipa mkopo wa usafiri ndani ya miaka mitatu na nusu baada ya kuwasili nchini Marekani.

Katika maandalizi ya kuondoka kwako, utapata pia uchunguzi wa matibabu kabla ya kuondoka. Hii itahakikisha kuwa una afya njema kusafiri na itasaidia wafanyakazi kuamua kama unahitaji msaada wowote wa matibabu ukisafiri.



## HATUA YA SITA: KUWASILI

Unapowasili nchini Marekani, mwakilishi wa shirika la uhamiaji (ama jamaa yako ukiwa na uhusiano wa kimarekani) atakutana nawe kwenye uwanja ya ndege. Shirika la uhamiaji linawajibika kukusaidia kwa huduma za kimsingi kwa siku zako za kwanza 30-90 nchini Marekani Utakuwa na haki ya kisheria na wajibu wa kufanya kazi nchini Marekani na Shirika la uhamiaji litakuunganisha na huduma za ajira. Ukiwa na watoto wa umri wa shule, wanaweza kuhudhuria shule za umma bila malipo wanapo wasili.





## BAADA YA UHAMIAJI

Baada ya mwaka moja Marekani ni lazima kutuma ombi kuwa mkazi halali wakudumu. Miaka mitano baada ya kuwasili unaweza tuma ombi kuwa raia wa Marekani na haki zote na majukumu ya Wamarekani wengine.

**Huduma zote za mchakato wa uhamiaji ni bure. Kwa wakati wowote katika mchakato haistahili mtu yeyote kuomba malipo kutoka kwako kwa huduma yoyote. Ikiwa mtu yeyote atakuitisha pesa, kukulazimisha kufanya ombi, kudai kuwa anaweza kuingilia kati au kuharakisha ombi lako, au kukutishia kwa namna yoyote, tafadhali ripoti hii kwenye Kituo chako cha Usaidizi wa uhamiaji.**

CORE Cultural Orientation Resource Exchange

The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**